# Dovutwa awalaumu UKAWA kususia Bunge

Na Rose Itono

CHAMA cha United People's Democratic (UPDP) kimelaani kitendo cha wabunge wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) kususia kujadili bajeti bungeni na kusema kuwa, mjadala wa kusitisha matangazo ya moja kwa moja ya bunge na uanzishwaji wa studio ya kurekodi na kurusha matangazo yake ulijadiliwa katika bajeti ya mwaka 2015/16 na wao walikuwepo.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa UPDP, Fahmi Dovutwa alisema kuwa,kukosekana umakini wa usikilizaji vikao vya Bunge kwa UKAWA kumejionesha wazi kwa hili kwani si jambo jipya kwao tayari lilishajadiliwa katika bajeti ya mwaka 2015/16.

Alihoji kama bunge limepitisha bajeti kwa ajili ya studio ya bunge ambayo UKAWA waliridhia uanzishwaji wake.

"Sasa wanachopinga ni nini au wanapokuwa wanajadili hawakujua maana yake?" Alihoji huku akisisitiza kwamba endapo uwepo wa UKAWA bungeni ungekuwa unazingatia kinachozungumzwa wasingeshangazwa kusitishwa kwa matangazo ya moja kwa moja.

Pia alizipongeza hoja za Freeman Mbowe na kudai ni za msingi na zimeiva kwa kutosha kuchangamana ndani ya Ukumbi wa Bunge, lakini kitendo cha kuondoka nazo nje inaonesha ni namna gani mfumo wa uongozi ndani ya UKAWA ni wa mtu mmoja na kwamba hautoi nafasi ya watu wengine kusikilizwa.

Alisema kuwa, pia inaonesha Ukawa wana udhaifu mkubwa wa kujenga hoja kwa kutegemea mazingira na wakati kwani kwa kitendo chao cha kutoka ndani ya Bunge kwa msimamo wa kugomea hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu inaonesha wazi ni namna gani serikali ilikuwa sahihi kusitisha matangazo ya Bunge ya moja kwa moja.

"Kwa sababu kodi za Watanzania haziwezi kuwa zinatumika kwa kufanya vibweka bungeni Watanzania wanatarajia wabunge waliowachagua watakuwa ni sauti ya kuwapigania mipango yao ndani ya bunge sambamba na kuwatetea pale itakapobidi," alisema Dovutwa.

Aliwataka UKAWA kubadilika kwa kuanza kutafakari zaidi badala ya kufanya siasa kwa historia.

"Kitendo chao cha kuondoka bungeni si cha kiungwana kwani kinawanyima nafasi wapigakura wao," alisema.

Alimtaka Spika wa Bunge kuwaeleza Watanzania vigezo vinavyowezesha wabunge wasiofanya kazi walipwe posho kwa kumshauri kuwaona kama wabunge hewa wasiostahili malipo yeyote.



*Baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni ya Vodacom wakifuatilia mada kuhusiana na usalama wakati wa semina ya kuadhimisha Siku ya Usalama Kazini Duniani iliyofanyika kwenye ofisi za kampuni hiyo Mlimani City, Dar es Salaam juzi. Na Mpigapicha Wetu*

## Wahamasishwa kupeleka watoto wapewe chanjo

Na Magreth Kinabo-(MAELEZO)

JAMII imeshauriwa kupeleka watoto wote wanaostahili kupata chanjo, walio chini ya umri wa miaka mitano, katika vituo vya afya ili waweze kupewa chanjo ya kutokomeza maradhi na kupunguza vifo vya watoto.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibun na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Dkt. Mpoki Ulisubisye wakati wa maadhimisho ya wiki ya chanjo nchini yaliyofanyika kwenye Hoteli ya Serena jijini Dares Salaam.

Alisema utoji wa chanjo hiyo umeaanza Aprili 25,mwaka huu na kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Kumilisha Chanjo,Epuka Ugonjwa wa Polio'.

Hivyo vituo vya kutolewa kutolea huduma za afya vinafunguliwa kuanzia saa 2: 00 asubuhi hadi saa 11.00 jioni.

"Kila mmoja wetu ana wajibu wa kuhakikisha mtoto wake, mtoto wa jirani mwingine yeyote anapewa haki ya chanjo ili kumzuia asipatwe na maradhi ambayo yanakingwa na chanjo au asiwe na hatari kwa wengine kwa kuwaletea ugonjwa," alisema Dkt. Ulisubisye.

Aliongeza kuwa chanjo ni mikakati mwafaka katika kutokomeza maradhi na kupunguza vifo vya watoto, hivyo hupunguza gharama kubwa ambazo familia zetu na taifa kwa ujumla lingetumia katika kutibu maradhi yanatokana na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Alisema chanjo huzuia takriban vifo milioni mbili hadi tatu kwa kila mwaka kutokana na maradhi yanayokingwa kwa chanjo duniani.

Aliyataja maradhi hayo kuwa ni Dondakoo, Surua ,Polio,Kifua Kikuu,Kifaduro,Pepopunda,Homa ya ini,homa ya uti wa mgongo, kichomi na kuhara.

# Asasi zatoa misaada kukomesha ujangili

Na Severin Blasio, Mvomero

ASASI ya kuhifadhi mazingira nchini, CONASU, kwa ushirikiano na Shirika la The Ruffor Foundation (RSG) la Uingereza, wametoa mizinga ya ufugaji nyuki yenye thamani ya sh. milioni 3.5 katika vijiji sita.

Ni vijiji vinavyopakana na hifadhi ya Mikumi mkoani Morogoro ili kukomesha ujangili wa tembo na uharibifu mazingira.

Akizungumza kwa nyakati tofauti kwenye vijiji vya Doma,Maharaka,Kihondo,Mkata,Kilangali na Palakuyo vilivyo wilayani Kilosa na Mvomero, Mratibu wa CONASU katika Mradi Shirikishi wa Hifadhi Tembo na makazi yake,Angelus Runji alisema njia hiyo inalenga kuwalinda wanyama na hifadhini kwa kuepusha ujangili na uharibifu mazingira.

Runji alisema,mizinga hiyo itasaidia kukuza kipato na kufanya wananchi waliopo maeneo hayo kuacha kujihusisha na ujangili na hususan katika hifadhi za taifa hivyo wanyama kama tembo na wengine wataweza kuongezeka kwa vizazi vijavyo.

Runji ambaye pia ni Mkurugenzi wa asasi hiyo alitaja faida za ufugaji nyuki mpakani mwa hifadhi na vijiji vyao hivyo kuwa ni njia rahisi ya kuwazuia wanyama hao wakiwemo tembo kutokana na kutopatana nao,zao la asali litokanalo na nyuki lina soko kubwa ndani na nje ya nchi na ni dawa kwa viumbe vyote duniani.

Akiunga mkono juhudi hizo Muikolojia wa Hifadhi ya Mikumi, Samweli Mgohachi alibainisha kuwa mpaka miaka ya 1980 Tanzania ilikuwa na zaidi ya tembo 600,000 ambapo kwa takwimu za karibuni inaonyesha ina tembo wanaokadiriwa kufikia 40,000 kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kasi ya uwindaji haramu uliopo.

"Mbali na kuwa shukuru mawazo mazuri ya asasi kama Conasu na mengine yenye mtazamo huu pia nikipongeze kijiji hiki kwa kazi kubwa kinayoifanya kuwanusuru hawa tembo, kwani ni kijiji pekee chenye sifa ya kutoa taarifa ya aina mbalimbali zinazoonesha kuhatarisha wanyama na wananchi kwa ujumla," alisema Muikolojia Samweli.

Kwa aupande wao Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkata wilayani Mvomero, Katheline Sebastian na Katibu wa Jumuiya ya Uhifadhi Mazingira na Wanyama Pori (KIDOMA), Daniel Gasper kwa nyakati tofauti walibainisha changamoto zinazowakatisha tamaa ya kushirikiana na TANAPA kuwa ni kukosa kifuta jasho licha ya kazi ngumu na ya hatari wanayoifanya dhidi ya majangili,wafugaji kuingiza mifugo hifadhini,wachoma mikaa na wapasua mbao.

Hata hivyo, Katibu wa Jumuiya ya Kidoma, Gasper mbali na kubainisha kushuka kwa ari ya wanakijiji kuimarisha ulinzi dhidi ya wanyama waliohatarini kutoweka akiwemo tembo,pia alisema juhudi zao za kukomesha uharibifu na ujangili unadhoofishwa na nguvu ya rushwa hasa kwa viongozi wa serikali na vyombo vya dola wilayani humo.

RSG/CONASU/2016

# Vitendo vya ubakaji vyatikisa Monduli

■ Wankyo Gati, Monduli

SERIKALI imeombwa kuingilia kati vitendo vya ubakaji kwani vimezidi kushamiri wilayani hapa mkoani Arusha.

Akizungumza kwa niaba ya wanawake wenzake, Jenipher John alisema hali si nzuri hususan kwa wananchi wa Kata ya Mto wa Mbu kwani wanawake wanateseka.

Jenipher aliweka bayana kilio hicho kwenye mkutano wa wananchi wa kata hiyo ambao ulishirikisha viongozi wa wilaya kuanzia ngazi ya mtaa.

"Wanawake tunaishi kwa wasiwasi kwa sababu vitendo vya ubakaji katika wilaya yetu vinaongezeka siku hadi siku, tunaomba Serikali itusaidie," alisema.

Wanawake hao walimweleza Mkuu wa wilaya, Francis Mitti wasiwasi wao kuhusu kushamiri kwa vitendo hivyo vya ubakaji.

Kwa upande wake, Mkuu wa wilaya alisema kuwa serikali italichukulia suala hilo kwa uzito mkubwa na kuvikomesha vitendo hivyo.

Alisema atarejesha amani amani katika eneo hilo na akinamama wataendelea na shughuli zao za kila siku bila hofu hasa eneo la Kata ya Migungani na viunga vyake.

Akijibu hoja za wananchi za kutopewa ushirikiano na Jeshi la Polisi wakati mtuhumiwa wa ubakaji anapobainika, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Charles Mkumbo alisema kama wana ushahidi wa kutosha wa askari yeyote ambaye hafuati maadili ya kipolisi waripoti kwake.



Mafundi ujenzi wa Kampuni ya Estim wakijenga mtaro wa barabara ya Morocco-Mwenge Dar es Salaam jana, inayopanuliwa kwa fedha sh. bilioni nne ambazo zilikuwa zitumike kwa ajili ya sherehe ya Uhuru iliyofutwa na Rais Dk. John Magufuli mwaka jana. (PICHA NA DOTTO MWAIBALE)

# TAT yakimbilia bungeni

■ John Banda, Dodoma

CHAMA cha Wasafirishaji Tanzania (TAT), kimeiomba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kukisaidia ili kuondolewa utitiri wa kodi wanazotozwa.

Kauli hiyo ilitolewa jana mjini hapa na rais wa chama hicho, Zakaria Hanspope wakati walipokutana na kamati hiyo.

Hanspope aliiomba kamati kuwasaidia kupunguza utitiri wa kodi wanaotozwa na taasisi mbalimbali kwani zimekuwa zikiwaumiza wafanyabiashara.

Alitaja changamoto wanazokabiliana nazo kuwa ni ulipaji wa kodi zitolewazo kwenye mizigo ya nje ambayo huchangiwa watoa huduma wa bandari."Kitu hiki kinatuumiza sana, gharama zitapanda kwa asilimia 18, jambo hili linaonekana katika Bandari ya Dar es Salaam tu... wengine wote wameikataa,"alisema.

Pia, alisema kuanzishwa wa himaya ya forodha ya pamoja (single customes territory) kumeleta athari kwa wasafirishaji wa nchini hivyo kuwapa nafasi wafanyabiashara wa nchi zingine kutumia bandari za Beira, Durban, Walves bay na Lobito inayokuja kwa kasi.

Makamu Mwenyekiti wa umoja huo, Omari Kiponza alihoji kazi ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwani wamekuwa wakiwaumiza kwa kukusanya kodi badala ya kufanya kazi ya ukaguzi wa bidhaa.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa kamati, Suleiman Kakosa alikiri msururu wa sheria umemfanya msafirishaji akimbie Bandari ya Dar es Salaam.

"Nawaahidi kuwasaidia kwani nyie mmeshika uchumi wa nchi ila zipo sheria zinahitajika kufanyiwa marekebisho, hilo tumelibeba na tutaishauri serikali," alisema.

# Bendera ahamasisha kilimo cha umwagiliaji

■ Julieth Peter, Babati

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Dk Joel Bendera amesema njia pekee ya kuwasaidia wakulima ni kilimo cha umwagiliaji.

Alitoa kauli hiyo mjini hapa jana katika mkutano wa wadau wa umwagiliaji ulioandaliwa na Shirika la World Vision Tanzania.

Dk Bendera alisema kilimo hicho kitawasaidia kuzalisha mazao mwaka mzima tofauti na ilivyo sasa.

Alisema Serikali inahamasisha kilimo cha umwagiliaji kwa sababu kina tija na kwamba kitamwezesha mkulima kuvuna mazao mengi na kuinua kipato chake.

"Sote tunatambua kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu lakini bila jitihada za pamoja hatuwezi kupiga hatua kwa haraka, wakulima wengi hadi leo wanategemea mvua ili waweze kulima na kilimo hiki kwa sasa hakina uhakika wa mavuno endelevu kutokana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Alisema mkoa huo una maeneo mazuri kwani una jumla ya hekta 36,882 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hivyo matumizi sahihi ya teknolojia yatasaidia kuleta mapinduzi.

Alizitaka halmashauri zote mkoani humo kutenga bajeti kwa ajili ya kuongeza rasilimali watu ya kutosha katika fani ya maofisa ugani na umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji.

Kwa upande wake, Frank Raymond akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa World Vision, alisema mradi wa Pivot Irrigation upo mikoa 12 ya Tanzania, lakini Manyara umekuwa wa kwanza katika mpango huo.

Alisema kuwa mradi huo una uwezo wa kumwagilia ekari 120 kwa pamoja na utawasaidia wananchi kuondokana na kilimo cha mvua.

# "Wananchi wana uelewa mdogo kutunza hifadhi"

■ Thadei Hafigwa, Morogoro

WANANCHI wanaoishi katika vijiji sita vinavyozunguka Hifadhi ya Wanyamapori Mikumi wana uelewa mdogo wa kutunza hifadhi hiyo.

Hayo yalibainika katika mkutano wa mashauriano baina ya wananchi na hifadhi katika kujengeana uelewa namna ya kuhakikisha makazi ya wanyama yanalindwa.

Mkurugenzi wa Asasi ya Conasa (Conservation of Nature for Survival), Angalus Runji alisema utafiti uliofanywa na taasisi yake katika vijiji hivyo umebaini kuna tatizo hilo.

Alisema utafiti uliofanyika katika vijiji vya Doma, Maharaka, Kihondo, Mkata, Kilangali na Palakuyo walibaini tembo wanatoka kwenye makazi ya hifadhi na kuingia vijijini.

Mkurugenzi alisema hiyo inaweza kusababisha wanyama hao kuuawa na wanavijiji.

Kutokana na hali hiyo, alisema asasi yake inashirikiana na Shirika la Ruffor Foundation (RSG) la Uingereza ili kuwapa elimu wananchi wanaoishi kandokando ya hifadhi na mbinu ya kuwalinda tembo.

Alisema walitoa mizinga 30 ya nyuki kwa wananchi yenye thamani ya sh. milioni 3.5 katika vijiji hivyo sita ili kukomesha tabia ya baadhi ya watu kuua tembo na uharibifu mazingira.

"Nyuki ni wadudu wakali lakini ni rafiki wa binadamu kutokana na kuwa na uwezo wa kutengeneza asali ambayo ni bidhaa muhimu kwa maisha ya mwanadamu, pia eneo lenye nyuki tembo hawawezi kupita ndiyo maana tumegawa mizinga hiyo," alisema.

Muikolojia wa hifadhi, Samweli Mgohachi alisema hadi miaka ya 1980 Tanzania ilikuwa na zaidi ya tembo 600,000 lakini takwimu za karibuni zinaonesha wamepungua hadi 40,000.

RSG/ CONASU /2016

# Foreign NGO helps community to protect elephants

**By Guardian on Sunday Correspondent, Morogoro**

MIKUMI National Park Authority has asked the community surrounding the park to support government efforts in conserving, protecting and managing elephants in the country.

Mikumi National Park Ecologist Samweli Mgohachi told a sensitization seminar conducted recently for villagers from six villages in Morogoro region.

Mgohachi said the community had an important role to play in ensuring protection and management of African elephants was successful.

"This initiative of raising awareness to villagers opens a new chapter in park-community shared objective of conserving Mikumi National Park," he said.

Organised by Conservation of Nature for Survival (CONASU) with support from the London-based The Rufford Foundation, the meeting gathered villagers from Kihondo, Maharaka, Doma and Mkata villages from Mvomero district, and Parakuyo and Kilangalai villages from Kilosa district.

Some villagers admitted that it was possible to end destructive practices which were being carried out in the park. CONASU Executive Director Angelus Runji said the sensitization meeting was one of the activities in the project to enhance the community's protection and management of African elephant habitat, which was underway in Mikumi National Park.

"We are also encouraging the community to involve themselves with some activities like beekeeping to raise their income at the same time protecting our animals," he said.

He said there was a need to have an ecological balance.

"That is why we have taught villagers to stop fire burning and charcoal making in forests in order to make beekeeping project possible," he said.

Already the organization has supplied 30 beehives worth Sh3.5million to six villages with a condition that the projects must be supervised by village authorities.

"We are sure that through enhancing community capacity, elephant habitat will be safe and secure and it will end poaching to the great extent.

Mkata village chairperson Catherine Sebastian and Secretary for Kidoma Community Conservation of Environment and Wildlife Daniel Gasper said they were facing various challenges in conserving the national park. They alleged that they were being let down by the Tanzania National Parks for not paying them anything despite the hardships they faced in dealing with poachers and pastoralists who entered the park for grazing their cattle.



**Institute of Tax Administration students listen to a speech by Tanzania Revenue Authority Acting Director for Human Resources and Administration Victor Kimaro (not in picture) during the institute's Students Career Day held in Dar es Salaam, yesterday. Photo: Mpoki Bukuku**

# Dons lay accent on competent teachers in govt schools

**By Beatrice Philemon**

ACADEMICIANS have urged the government to ensure that it employs quality teachers to enable them impart required skills and knowledge to students of all levels of education.

They said teachers need also to be assessed their language knowledge in terms of speaking, reading, writing and listening before being employed to teach in public schools.

"A lecturer with the School of Education of the University of Dar es Salaam, Dr Mwajuma Vuzo, said at the just-ended Seminar on Teaching and Learning in Mother Tongue held at the institution that there is need for the government to employ competent teachers if it is to raise the standards of education in the country.

She suggested teachers to be assessed in their respective areas of studies periodically, especially in English subjects to know their competence and improvements in their careers.

According to her, a number of students were not performing well in the subject because of lack of specialized teachers in the subject at all levels of studies.

"With good teachers, students at all levels will always perform well," she underscored, adding:

"English language has a lot of benefits, not only to the nation but also around the globe. We therefore need to ensure our students are capable of speaking the language."

Commenting on the debate, Prof Kitila Mkumbo, Department of Education Psychology and Curriculum Studies at the university said stressed the importance of ensuring that children are knows their mother tongue.

"It is very important for children to learn other languages, but a mother tongue is equally important because it identifies us"

However, he said there was need also to ensure that English language is introduced at an early stage of learning to make students gain confidence in their studies.

"English is a survival language, we need to be serious on this subject because children are poorly performing in their studies and this is a big problem in the country" he said.

He added, "If our neigbouring countries can learn English, so we can do better."

A recent research by Twaweza East Africa on challenges children face from primary and secondary schools in the country shows at least 63 percent of parents are of the views that English should be used as a medium of instruction at all levels of studies.

The research also suggested that the key to improving the quality of primary education is to focus on teachers.

Other suggestions of the report touched on improving education in terms of follow up on teacher performance, increase teacher's salaries and number of teachers.

# Ministry hosts dialogue with bankers on land loans

**By Devota Mwachang'a**

MINISTER for Lands, Housing and Human Settlements Development William Lukuvi has asked financiers and supporters of agriculture to ensure that loans issued to farmers are solely used to boost the agricultural sector.

He was speaking in Dar es Salaam recently at a meeting with bankers and land stakeholders.

The minister said if people invested in farming in accordance with the promotion of the sector, the country would be at a better position of sustainable development depending on agriculture.

He cautioned loan applicants against using land title deeds as collateral for their loans and then use the money to undertake other businesses, saying farmers needed instead to ensure their farming land was properly developed for the country's economic well-being.

"Banks and other agricultural loan financers need to make follow-ups to ensure the issued loans are used for the intended purposes," he said.

According to him, many people owned big plots which were not secured, saying more than 200,000 acres of farming land were mortgaged with banks as as guarantees for loans.

"Farmers need to use their customary land certificates to process bank loans for their farms because they are recognized by the government," he said.

Currently, 360,000 farming land certificates have been issued to farmers countrywide.

For her part, title deed registrar Subira Sinda blamed financial institutions for issuing loans to applicants without verifying the legitimacy of the land deeds submitted by the applicants.

"It is better for them to ensure that the documents are original before issuing loans, instead of only relying on security forms which have been filled by the applicants," she said.

Programme Coordinator of the Property and Business Formalisation Programme (Mkurabita) Seraphia Mgembe said bankers have the responsibility to building the capacity of people to utilize their land certificates to secure loans and thus improve their incomes.

"Loan beneficiaries lack enough awareness on how to utilize their loans as intended, eventually they fail to repay the loans...so they need education," she said.

Tuse Joune, acting director Tanzania Bankers Association, applauded the minister for his idea of meeting bankers for dialogue, saying the dialogue would help resolve issues before resorting to courts of law.